Antonio Rosmini

# MAADILI YA UKAMILIFU WA KIKRISTU



Edizioni Rosminiane
Stresa – VB (Italia)
2020

Antonio Rosmini

# *Maadili ya ukamilifu wa Kikristu*

Edizioni Rosminiane – Stresa 2020

Original Title: *Maxims of Christian Perfection*,
Edizioni Rosminiane – Stresa, VB, Italia
Translation by Firmati Tarimo.
Matini ya Maandiko zimetoka *Biblia ya Kiafrika*

# Yaliyomo


Mwenyeheri Padri Antonio Serbati Rosmini (1797-1855)....... 7

Dibaji ........................................................................ 8

Mafundisho ya Kiroho ................................................ 9

KANUNI ZA UKAMILIFU:
Juu ya Njia ya Ukamilifu kwa Ujumla ....................................... 11

KANUNI YA KWANZA:
Kutamani Tu na Bila Kikomo Kumpendeza Mungu yaani kuwa Mnyofu/Mtakatifu/Mwenye Haki. ................................ 15

KANUNI YA PILI:
Kuelekeza Mawazo na Matendo Yote kwa Ongezeko na Utukufu wa Kanisa la Yesu Kristo ........................................... 19

KANUNI YA TATU:
Kuwa na Amani na Utulivu bila Mahangaiko Kufuatana na Mipango ya Mungu Kwetu au kwa Kanisa la Yesu Kristu na Kufanya Kazi kwa Ajili ya Kanisa ........................................... 23

KANUNI YA NNE:
Kujiweka Kabisa na Kikamilifu katika Mpango na Maongozi ya Mungu ........................................................... 25

JUU YA KANUNI YA TANO:
Kuungama, na Kukiri kwamba Mimi Si Kitu Mbele ya Mungu, ni Bure ........................................................... 33

Juu ya Kanuni ya Sita:
Kuyaongoza Matendo yote ya Maisha kwa Roho wa Ufahamu (Roho Wa Akili) .......... 37

Nyongeza
Wasifu wa Mwenyeheri Padri Antonio Rosmini .......... 44

## Mwenyeheri
# *Padri Antonio Serbati Rosmini (1797-1855)*

Antonio Serbati Rosmini alizaliwa tarehe 24 Machi 1797 huko Rovereto kaskazini mwa Italia. Alibatizwa tarehe 25 Machi 1797.

Anaitaja siku ya kubatizwa kwake kama siku yake ya kuzaliwa. Kisha anaienzi siku hii sana na kumshukuru Mungu kumchagulia siku hii bora ya kupashwa habari Bikira Maria.

Katika maisha yake alikuwa na ibada ya dhati kwa Bikira Maria Mama yetu wa Mateso. Antonio Rosmini ni mwanzilishi wa Shirika la Mapendo (Warosmini 20.02.1828) na la Masista wa Maongozi (Sisters of Providence).

Antonio Rosmini aliandika vitabu vingi (jumla vitabu 97) katika uhai wake; baadhi yake kikiwa hiki cha msingi wa mwenye kutaka kufuata ukamilifu. Vipo vingine kama vile, Madonda Matano ya Kanisa Takatifu, na Mkusanyiko wa Mafundisho kwa Mapadri. Antonio Rosmini alikufa tarehe 1 Julai, 1855. Kabla hajafa na kwa vile alikuwa mkuu wa watawa Warosmini, Padri mmoja alimwuliza: «Baba Rosmini, tutafanya nini bila wewe», Rosmini alijibu, (adorare, tacere, godere) yaani, abudu, tafakari.

Antonio Rosmini aliwaachia wanawe mwongozo wa maisha yaliyojengwa katika upendo – pendo lisilochagua humfikia jirani na kumsaidia kiroho, kiakili na kimwili. Katika mgawanyo wa mapendo haya lile la kiroho ndilo la juu zaidi.

Antonio Rosmini alitangazwa mwenye heri na Baba Mt. Benedikto XVI tarehe 18.11.2007 na sikukuu yake huadhimishwa Julai 1 kila mwaka, siku aliyozaliwa katika ufalme wa mbingu.

Hatimaye twafariji ka na kufurahi kuwashirikisha utajiri wa mwanzilishi wa shirika letu.

*Pd. Firmati C. Tarimo, IC Provincial*

# *Dibaji*

Kitabu hiki ambacho kimewahi kuchapishwa kwa lugha mbali mbali, kiliandikwa kwa mara ya kwanza na Padre Antonio Serbati Rosmini huko Roma, Italia 1830. Toleo la kwanza kwa lugha ya Kiingereza lilikuwa 1887, na kurudiwa 1948 na 1962.

Tafsiri hii kwa lugha ya Kiswahili ni la kwanza na limetokana na toleo jipya kwa lugha ya Kiitaliano lililochapishwa na Città Nuova, Roma Italia 1976.

Rosmini ameziona Kanuni za Ukamilifu wa Kikristu kuwa msingi imara wa maisha yake na maisha ya wale watakaofuata katika kujitoa kwa Mungu, wawe watawa au watu katika maisha au wito mwingine wowote. Hii ni kwa sababu kinafundisha jinsi mtu anavyoweza kuelekeza na kupanga mambo ya maisha kadiri ya mpango wa Mungu, ambaye ndiye wema wa juu sana tunaotafuta na ni kwake tunaweza kupata utimilifu.

Baba Mtakatifu Yohana wa XXIII, alitumia kitabu hiki katika mafungo yake ya kujiandaa kuadhimisha miaka 80 tangu kuzaliwa kwake. Mwisho wa mafungu Baba Mtakatifu Yohana XXIII aliandika, «natamani kuwa mwema na mtakatifu kama njia pekee ya kumpendeza Mungu».

Ni matarajio yetu makubwa kuwa tafsiri hii ya kwanza kwa lugha ya Kiswahili itawasaidia wengi wa nyakati zetu kutamani zaidi na zaidi kuishi mafundisho ya Injili.

Mafundisho ya Kiroho

«*Bwana ndiye aliye fungu langu. Nimesema kwamba nitayatii maneno yako*» (Zab. 119 (118):57).

## Kanuni za Ukamilifu

# *Juu ya Njia ya Ukamilifu kwa Ujumla*

1. Wakristo wote, wafuasi wote wa Yesu Kristo, katika hali yoyote au mazingira yoyote watakayo jikuta, wanaitwa kuwa wakamilifu, kwa vile wote wanaitwa kufuata Injili ambayo ni kanuni ya ukamilifu. Na kwa wote ilisemwa na Bwana «Basi ninyi mtakuwa wakamilifu kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu» (Mat 5:48).

2. Ukamilifu wa Injili umo katika kushika kwa ukamilifu amri mbili za *upendo* – Upendo kwa Mungu na upendo kwa jirani. Kwa hiyo hamu ambayo Mkristo anasikia, na bidii anazofanya, ili kuunganika na Mungu na mapensi yake yote na katika matendo yake, kwa kadiri inavyowezekana katika haya maisha, ipo katika kutii amri iliyotolewa kea maneneo haya. «*Akamwambia, umpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote na kwa akili yako zote. Hiyo ndiyo amri kuu, tena ya kwanza. Na ya pili ni sawa na hiyo, umpende mwenzako kama unavyoipenda mwenyewe*» (Mat 22:37-39).

3. Ili kufikia ukamilifu huu wa mapendo ambao kila mfuasi wa Yesu Kristu lazima adhamiriae. Kuna njia mbalimbali, mojawapo ni maisha ya wakfu. Wanaochagua maisha ya wakfu au maisha ya utawa hujifunga kwa nadhiri tatu za. umaskini, useja (usafi wa moyo) na utii. Lakini hizi sio amri zinazowafunga Wakristu wote; bali tu ushauri unaotolewa na injili, kama msaada kuondoa kutoka katika akili, moyo na maisha ya Mkristo, kila kikwazo ambacho kingemzuia katika kujifungua kabisa na kuwa tayari kumpenda

Mungu na jirani. Nadhiri hizi tatu siyo lengo la maisha ya utawa, ni nyenzo zinazosaidia kumweka huru zaidi yule anaye ziungama ili kwa kufanya a mpenzi ya Mungu ambayo ni amri ya mapendo.

4. Kuungama haya mashauri matatu (au kwa maneno. mengine kuweka hizi nadhiri tatu) kunafanya kitu kinachitwa ukamilifu wa utawa – kitu ambacho sio cha kawaida kwa Wakristo wote, lakini kinachofaa kwa wale ambao wanajitoa zaidi na wenye kuwa tamaa na bidii ya ufuasi wa Yesu, ambao kwa kweli wanajitenga wenyewe na utajiri, starehe na kwa hiari yao wenyewe kuwa huru zaidi kutoa utashi wao wote kwa Mungu na Kwa jirani.

5. Mtawa, yaani Mkristo anayeungama nadhiri tatu za umaskini, useja na utii, anapaswa kuzitumia kiadilifu kwa njia ambayo atajenga ule ukamilifu wa mapendo ambao yeye anaitwa pamoja na Wakristo wenzake wote.

6. Kwa hiyo, Mkristo ambaye ingawa haweki hizi nadhiri tatu lakini bado anataka sana kufikia ukamilifu wa mapendo ya Ki-Mungu ambao kwao anajitoa kabisa na ambao kwao ameitwa na Mungu katika ubatizo, ya mpasa kuwa mwangalifu sio tu katika kutokuumbwa, kuvunja heshima, kukashifu hizi nadhiri (zoezi la kuishi hizi nadhiri) kama asemavyo Thomas wa Aquina (Summa, II, II CLXXXVI, II,). Lakini pia ya mpasa kutambua na kufahamu ubora, uzuri, na wema wake na azipende. Hivyo anapaswa kutamani kuwa na ukarimu wa Roho na kuelewa ukweli unaomsukuma mtu kutumia njia zinazofaa kuuweka huru moyo wake kutoka katika maangalizi na makwazo yanayomzuia asielekeze maisha yake yote kwa Mungu kwa upendo. Mtu ambaye siyo Mtawa anaweza wakati mwingine kushawishika kutothamini sana nadhiri hizi kwa sababu ya ubinafsi ambao kwa kawaida humfaya mtu akose ukarimu wa kujitoa kwa Mungu na jirani. Ni kwa unyenyekevu tu ambao utampatia ufahamu juu ya nafsii yake, kama mmoja ambaye, hali yake katika ufalme wa Mungu ni ya thamani thamani na heshima, kama vile ilivyo kwa Mtawa.

7. Upendo kamili, ambao ndio ukamilifu wa Ukristu, una–muunganisha mtu na muumba wake. Ni kama kujiweka wakfu, au kujitoa sadaka kwa Mungu kwama vile kuiga mafano wa Mwana wa Pekee wa Mungu. Kwa kujiweka huku wakfu, mtu anaamua kutokuwa na malengo mengine katika matendo yake zaidi ya kumwabudu Mungu, na kutokuwa na makusudi mengine wala kutotafuta jema lingine lolote au furaha zaidi ya ile ya kumtumikia na kumpendeza Mungu.

8. Kwa hiyo, Mkristu wa kweli anayetaka kulenga ukamilifu ambao kwao ameitwa, anapaswa kuamua kila wakati kutafuta katika kila tendo la maisha yake kile anachoamini kuwa kinapendeza zaidi Mungu, na kinafaa zaidi kwa utukufu Wake na kulingana na mapenzi Yake.

9. Ili kuweza kujua ni nini katika maisha ya kila siku kinalingana na mapenzi ya Mungu, na hivyo kitu bora kabisa kufanya, Mkristu anapaswa kuweka mbele yake, na kutafakari siku zote kiini cha maongozi ya Mungu. Kweli Wakristu wote wamepewa nyenzo za ukamilifu. Ila ikumbukwe kuwa wale waliochagua maisha ya utawa wanayo nafasi zaidi ya kutumia nyenzo hizi na hivyo kwake yeye aliyepewa zaidi, kwake itatakwa zaidi.

10. Mafundisho haya, na kwa kweli Injili yote inaweza kufupishwa katika mafungu mawilii; kwanza, madhumuni ama lengo la matendo yetu, ambalo Mkristo anapaswa kutilia maanani kila wakati ili aweze kufuata kwa upole wa njiwa. Kwa sababu hiyo ni vizuri lengo la maisha ya Ukristu liwe wazi na dhahiri. Pili, njia anayopaswa kutumia, na maarifa, ujanja kama wa nyoka, katika kufikia lengo.

## Angalisho

1. Ukamilifu wa Ukristu:

- Ni wito wa Bwana wetu Yesu Kristu kwa kila mmoja katika hali yoyote ile ya maisha (rej. Mt 5:48).

- Huonekana na kukamilika katika amri kuu ya Mapendo (rej. Mt 22:37-39).
- Mfano wa Ukamilifu wa Ukristu upo katika Bwana wetu Yesu Kristu aliyekuwa mtii kwa mapenzi ya Baba mpaka mauti ya Msalaba.
- Upo katika kuiga mfano wa Bwana wetu Yesu Kristu, siyo tu kwa kutii mapenzi ya Baba, bali pia ambaye maneno na matendo yake yote aliyaelekeza katika utukufu wa Mungu.
- Wakati wote, pamoja na Yesu kufanya mapenzi ya Mungu. Ndiyo kusema mawazo, maneno na matendo ya Mkristu yawe kama atakavyo Mungu. Huu ndio utukufu wa Mungu.

Kanuni tatu za mwanzo ndio *lengo*, kanuni tatu za mwisho ndio *njia* ya kufikia lengo.

Kwa hiyo kuna kanuni sita ambazo ni:

1. Kutamani tu na bila kikomo kumpendesa Mungu yaani kuwa mnyofu, mwenye haki[1].
2. Kuelekeza mawazo na matendo yetu yote kwa kuongoezeka na kwa utukufu wa Kanisa la Yesu Kristu.
3. Kuwa na Amani na utulivu bila mahangaiko kufuatia yote yanayotokea kufuatana na mipango ya Mungu kwetu au kwa kanisa la Yesu Kristu.
4. Kujiweka kabisa na kikamilifu katika mpango na maongozi ya Mungu.
5. Kuungama, kukiri na kukubali kwamba mimi si kitu, ni bure bila Mungu.
6. Kuyaongoza matendo yote ya maisha kwa roho na ufahamu (Roho na akili).

Hizi kanuni sita zinaunda somo la mafundisho yaitwayo Kanuni za Ukamilifu wa Mkristu.

---

1. Neno haki limetumika hapa kumaanisha bila dhambi na halihusiani na mambo ya kimahakama hata kidogo.

## Kanuni ya Kwanza

## *Kutamani Tu na Bila Kikomo Kumpendeza Mungu yaani kuwa Mnyofu/Mtakatifu/ Mwenye Haki*

1. Wote wanaompenda Mungu kwa jinsi ilivyoelekezwa katika Injili «Kwa moyo wao wote, na kwa roho yao yote na kwa akili yao yote» kwa vile hawawezi kumpa Mungu kitu chochote kizuri, kwa sababu Mungu ana kila kizuri, wanatamani walau kuwa wanyofu mbele zake, kwa kubali/ukamilifu wake usio na kiasi, na kwa kumtolea katika kila wanalofanya, utii wa hali ya juu inavyowezekana, heshima/ibada kujitolea na kumwabudu. Hii maana yake nikuwa, wote wanaompenda Mungu wanatamani tu na bila kikomo utukufu wake. Ukamilifu wa Kikristu unamaanisha na jumuisha bidii katika kufikia utakatifu wa hali juu inaowezekana.

2. Hivi heshima ya juu kabisa ambayo mtu anaweza kumpa Mungu iko katika kujinyenyekeza nafsi yake na kutamani tu mapenzi yake yalingane na kuendana na mapenzi ya Mungu. Hivyo Mkristu wakati wote ange penda na amejiandaa kuchagua chochote kinchompendeza Mungu kuliko kitu kingine chochote. Hii ni kwa sababu moyo wa Mkristu unalenga tu katika kumtamani Mungu inavyowezekana na kuliko yote.

3. Na kwa vile kinchotufanya towe wa thamani zaidi mbele ya Mungu ni haki, kumbe basi Mkristu yampasa kuendelea kuomba afanyike mnyofu zaidi na zaidi na mtakatifu siku baada ya siku. Ni lazima awe na hamu ile isiyo na kikomo wala kutosheka katika hili,

na aendelee kusali zaidi na zaidi akiomba hili, akisadiki kwamba atakuwa wa thamani zaidi kwa Mungu. Kadiri anavyoomba kuwa mnyofu/mtakatifu – atafarijiwa na maneno: «*Heri walio na njaa na kiu ya uadilifu maana hao atashibishwa*» (Mt 5:6). Kwa hiyo kwa yeyote anayekiri kuwa Mkristu, mambo yote yamepunguzwa katika hoja moja: kutamani kila wakati kuwa mnyofu zaidi kuliko alivyo sasa, na kusali kwa ajili ya utakatifu wake, kila wakati na bila kikomo. Lengo la kusali hivi ni kuwa kitu kimoja na Kristu, muungano wa karibu kama ule wa Yesu na Baba yake.

Hivyo basi hatapumzika, hatatosheka wala kuogopa kuwa anaomba mno kupita kiasi, yambidi ajikabidhi kwa wema usiopimika wa Mungu Baba ili ashibishwe, atoshelezwe na utajiri wa kiroho utokao katika hazina kuu ya Mungu isiyo na kipimo. Mungu atajua jinsi ya kufanya hili, na atalifanya hadi hapo mwombaji atapofanywa kuwa kitu kimoja na Mungu Baba:

a) Bwana wetu Yesu Kristu anatuhakikishia hili pale asemapo «*Mkimwomba Baba kitu, atawapa kwa jina langu*» (Yoh 16:23). Yesu kwa mfano wake akampa moyo Mkristo kufanya hivi.

b) Kwani kwa kiasi chochote cha utakatifu anachotaka kumwomba Baba yake wa Mbinguni, yampasa kufahamu Kristu amekwishaomba kwa sala ambayo haiwezi kusindwa kusikilizwa; nani juu ya utajatifu huu unaopatikana na sala hii ya Yesu, ambapo Kristu ameanzisha Kanisa la wateule ambalo halitaharibika.

4. Ifuatayo ni sala ya Yesu ambayo ni lazima impe moyo Mkristu kumuomba Baba i l i azidi kufanywa mtakatifu: «*Mimi ndani yao, nawe ndani yangu, ili wawe kamili katiku umoja, na ulimwengu utambue ya kuwa ni wewe uliyenituma, na umewapenda hao kama ulivyonipenda*» (Yoh 17:20-23).

5. Basi mfuasi wa Yesu ni lazima aendelee kutamani utakatifu, mpaka ifikie kwamba amememzwa katika mapendo, na anawcza kusema kama mtakatifu Paulo «*Si mimi tena ninayeishi hali ni Kristu anayeishi ndani yangu*» (Gal 2:20).

6. Kumbe hii hamu ya kuwa mtu wa haki isiyo na mipaka wala kipimo lazima nyofu na ya kutoka rohoni. Mkristu anaweza kufikia ukamilifu kwa kuvumilia na kudumu katika kuomba ombi hilo. Akijitahidi akili yake isisongwe sana na mambo ya nje, akiingia katika utulivu wa wa ndani (utulivu wa rohoni). Akiwa katika tafanario ya namna hii, yampasa aombe bila kuchoka ili aendelee kudumu katika hali hiyo kama Yesu navyomshauri, «*Basi kesheni na kusali daima*» (Lk 21:36). Ni lazima ajichunguze na kuona kama hiyo hamu aminifu, wazi na huru hivyo kwamba katika yote na katika mazingira yoyote atakayojikuta analenga tu kupata utakatifu, kufanyika matakatifu zaidi, mwenye haki zaidi, wa thamani zaidi kwa Mungu, na anayependekeza zaidi mbele ya Mungu.

7. Mkristu huyo asishangazwe hata kidogo wala asizitishe biddi zake kama ikiwa mambo ya dunia bado yanamvuta. Badala yake ajikusanye kwa mara nyingine tena, na afanye upya katika moyo wake, nia ya kuwa mtakatifu kamili, mpaka itakuwa kwamba hana hamu na kitu kingine chochote duniani, kikubwa au kidogo, isipokuwa tu kama kinaeelekeza katika unyofu, ndiyo kusema afanye lile linalompendeza Munzu zaidi.

8. Mkristo anapaswa kuelewa (ingawa sio rahisi), kwamba mambo yote lazima yawe chini na yakisaidia hii nia moja ya kuwa mtakatifu kamili. Kwa maneno mengine, hamu ya kitu chochote basi itokane na uwezo wa hicho kitu kumfanya mtakatifu zaidi, na sio kwa sababu kina thamani chenyewe zaidi ya hiyo

9. Na kwa kuwa utakatifu unakuja mara moja kutoka kwa Mungu na hakuna chanzo kingine, Mkristo yampasa asiwe na mapenzi kwa kitu chochote isipokuwa kama anajua kwamba ni njia iliyochaguliwa na Mungu kwa utakatifu wake. Yampasa awe mwangalifu ili asifikiri (kama inavyotokea mara nyingi) kwamba hii hali halisi (kama ilivyosemwa katika sentensi iliyotangulia) kumbe kwa kweli anavutea na mapenzi yasiyofichika aliyo nayo kwa kitu kingine.

10. Badala yake, yampasa ashawishike kwa nguvu na kukubali vitu vyote katika mikono ya Mungu vyaweza kuwa nyenzo zinazofaa kama nyingine katika mipango ya Mungu; na kwamba kwa kawaida Mungu anapendezwa kuonyesha uwezpo wake kwa kutumia nyenzo zake katika kuendekeza mipango yake. Vitu ambavyo kufuatia maumbile yake vingekuwa vya mwisho kutumika. Mkristu asifikie uamuzi juu ya mambo hayo mpaka pale Mungu atakapomuwekea wazi mapenzi yake juu ya mambo hayo.

11. Na kwa kuwa Mkristu ana tamaa ile isiyo na mpaka wa kuwa na thamani mbele ya Mungu, anataka kwa ajili yake kila kilicho kweli kizuri, kwa kuwa hawezi kuwa wa thamani mbele ya Mungu bila kutaka kwa ajili yake kila kicho kizuri. Hivyo inakuwa kwamba hii tamaa inabeba tamaa zote nzuri, hivyo kumbe mtu yeyote mwenye hii tamaa kuu anatami pia wolovu wa binadamu wengine, latika njia inayompendeza Mungu.

## Kanuni Ya Pili

# *Kuelekeza Mawazo na Matendo Yote kwa Ongezeko na Utukufu wa Kanisa la Yesu Kristo*

1. Tamaa ya kwanza ya Mkristu ambaye moyo wake umejengeka katika utakatifu ni ile ya ongezeko na utukufu wa Kanisa la Yesu Kristo. Yeyote anayetamani utakatifu, anatamani pia utukufu wa Mungu vile inavyowezekana. Atatamani pia vitu vyote ambyo ni vya thamani mbele ya Mungu. Hivi anapendezwa na waamini wanaoshiriki kujenga ufalme wake hapa duniani.

2. Hivyo, Mkristu hatakosea kama atafanya kanisa zima kuwa ndio lengo la mapenzi yake, lengo la mawazo yake, matakwa yake na matendo yake, kwa kuwa anajua kwa hakika kwamba Mungu anataka Kanisa la Yesu Kristu liwe ndio njia kuu ambayo kwayo Jina Lake takatifu litatukiuzwa kikamilifu.

3. Mkristu anaweza awe hana hakika kwamba labda Mungu anataka kufanya kitu chochote maalum kama njia ya utukufu wake. Lakini hatakuwa na wasiwasi kuwa kanisa zima ni chombo na njia maalum zaidi ya ambayo kwayo Mungu atatukuzwa mbele ya viumbe vyote vyenye utashi.

4. Asingekuwa na hakika hivi kama ingekuwa ni kuhusu sehemu isiyo muhimu ya (Mwili mzima) Kanisa takatifu. Mapenzi yake ni lazima yatolewe kwa mchumba kamili wa Yesu Kristu,

lakini sio kwa kitu chocliote ambacho kinaweza kufanya sehemu yake lakini hakijaonyeshwa na Mungu kuwa ni sehemu kweli ya kanisa. Kwa kifupi; asitoe upendo usiopimika wala usio na mipaka kwa njia au kitu chochote mahususi, ambacho chaweza kudhaniwa – na kama Mungu anataka kinaweza kikawa kinafaa kwa utukufu wake. Kwani nani anajua labda Mungu ambaye njia zake zimefichika machoni petu na mwetu anaweza akakikataa au akaikubali? Lakini tunaposhughilika na Kanisa zima hakuna nafasi ya kuwa na wasiwasi wala mashaka. Kanisa limechaguliwa nay yeye na haitabadilika, kama nyenzo kwa utukufu wake, sasa na milele. Kwa hiyo basi, kwa Mkristu anayeazimia kufuata wito wake na kufuta utakatifu, kama anadiriki kutafuta katika maombo yote utukufu wa Yesu Kristu tu, yampasa kwa uwezo wake wote kuliweka Kanisa mbele ya mambo yote. Ni lazima kujikana kwa ajili ya Kanisa na kukubali kumwaga damu kwa kufuata mfano wa Yesu Kristo na wa watakatifu mashahidi.

5. Kanisa takatifu la Yesu Kristo lina sehemu tatu: Moja, ambalo liko katika safari ya mahujaji hapa duniani – kanisa lililo vitani (bado linashindana na kupigana). Mbili, ambalo linakaribia kituo chake mbinguni - Kanisa linaloteseka, lililoko toharani; na tatu Kanisa ambalo limeshafikiea makao yake mbinguni – Kanisa mshindi. Mkristu anajua kuwa kundi la kwanza na la pili litadumu kadiri ulimwengu utakavyodumu. Kanisa mshindi litadumu milele. Sehemu zote tatu zomechaguliwa kama njia na mahali pa kuishi utukufu wa Mungu ndani ya Yesu Kristu, kichwa na mtawala. Kwa hiyo, kama mwanachama wa jumuiya hii tukufu, Mkristu lazima kila wakati awe na upendo usio na mipaka kwa sehemu zote tatu na atake kutumikia na kumwaga damu yake kwa ajili yake.

6. Anafahamu kutoka katika maneno ya Yesu kwamba Kanisa la hapa duniani limejengwa juu ya mwamba ambao nguvu za kuzimu hazitalishinda. Mwamba huu ni Mtakatifu Petro, kichwa cha mitume, na waandamizi wake: yaani Kuhani Mkuu wa Roma (Papa) na maaskofu ambao ni mawakili wa Yesu Kristo hapa duniani. Kwa

kujua ukweli huu na kwa ufunuo wa Ki-Mungu kwamba, ofisi ya Roma imechaguliwa na mwanzilishi wa Kanisa, haitaweza kushindwa, kwa sababu tunaweza kusema pia kwamba kwa kuchaguliwa huku Roma imekuwa sehemu muhimu ya Kanisa la Yesu Kristu. Kwa hiyo ni wajibu kwa Mkristu kulea katika nafsi yake upendo usio na mipaka, mshikamano, na heshima kwa ukuu mtakatifu wa Askofu wa Roma. Upendo wake kwa hii sehemu muhimu ya mchumba safi wa Kristo ni lazima usiwe na mipaka, na yampasa kufanya bidii katika kila njia kuendeleza na kuenzi sehemu hii tukufu ya Mchumba Safi wa Yesu Kristu.

7. Mkristu mwaminifu atakodolea macho na kutamani uzuri na ukamilifu wa ile sehemu ya Kanisa ambayo imeshafika maskani yake. Ni lazima aamshe ndani mwake, na aendelee kuimarisha katika moyo wake hamu kwamba wana wa Kanisa au kwa kiasi chochote, wale wote ambao tangu mwanzo wamechaguliwa na kupangiwa na Mungu, wafikie utimilifu. Atatamani ujio wa ufalme kamili wa Yesu Kristu, ambao utamzunguka na hivyo kukamilisha utukufu na ushindi wake daima na milele. Kwa kuwa huu ndio mpango wa upendo wa Mungu na kwao Mungu anapendekezwa tangu mwanzo, ni lazima uwe pia, kamna ulivyo kusudi la mapenzi ya Mungu, kusudi kuu la nia zote za Mkristu.

8. Lakini kusudi hili haliwezi kufikiwa mpaka imekuwa kwamba mambo yote ya dunia yameisha, na Mkristu mwenyewe amekufa na mwili wake umerudia mavumbini ulikotoka, mpaka ulimwengu wote utakapoharibiwa na kuhukumiwa. Kwa hiyo Mkristu atatamani hali hii pia kwani anajua ndio jinsi iliyoteuliwa na Mungu ili kufikia ukamilifu wa utukufu wa Ki-Mungu na ushindi mkuu wa Yesu. Katika kila anachofanya ataweka maanani utukufu wa mbinguni kwani mambo mengine yote ni ya muda mfupi na yanapita upesi. Mkristu akumbuke na kutambua kuwa kifo ndio njia pekee ya kufikia pumziko la milele.

9. Kwa hiyo ataishi kana kwamba siku yoyote angepaswa kuacha mambo yote, kana kwamba atakufa wakati wowote.

Hataweka mipango na maandalio kwa ajili ya baadae, ila atasikiliza ndani mwake maneno ya Bwana wetu Yesu Kristu: «*Viuno vyenu na viewe vimefungwa na taa zenu ziwe zinawaka, nanyi iweni kama watu wanaomngojea Bwana wao, atakaporudi kutoka arusini, ili atakapokuja na kubisha, wamfungulie mara. Heri watumwa wale, ambao bwana wao ajapo atawakuta wanakesha. Amini nawaambieni, atajifunga na kuwakaribisha chakulani, atakuja na kuwahudumia. Na akija zamu ya pili au akija zamu ya tatu, na kuwakuta hivi heri watumwa hao. Lakini fahamu neno hili kwamba mwenye nyumba angalijua saa atakayokuja mwivi angalikesha wala asingaliiacha nyumba yake kuvunjwa. Nanyi jiwekeni tayari, kwa kuwa saa msiyodhani ndipo ajapo mwana wa Adamu*» (Lk 12:34-40).

## Kanuni ya Tatu

# *Kuwa na Amani na Utulivu bila Mahangaiko Kufuatana na Mipango ya Mungu Kwetu au kwa Kanisa la Yesu Kristu na Kufanya Kazi kwa Ajili ya Kanisa*

1. Yesu Kristu ana uwezo juu ya vitu vyote, vya mbinguni na vya duniani na amestahili kuwa Bwana wa wanadamu wote. Ndiye pekee anayeongoza kwa hekima, uwezo na wema matukio yote kwa busara isioelezeka, kufuatana na furaha yake, kwa ajili ya manufaa ya wale aliowachagua wanaofanya sehemu ya mchumba wake, yaani Kanisa.

2. Kwa hiyo Mkristu lazima awe na amani na utulivu akijawa na furaha wakati wote, akitumaini kwa Bwana wake, hata kama mambo yanaonekana kwamba ni kinyume, tena yanapingana na mafaa na manufaa ya Kanisa lenyewe. Hata hivyo asiache kusali na kumuomba Mungu ili mapenzi yake yatimizwe hapa duniani kama ilivyo mbinguni – Yaani watu washike amri yake takatifu ya mapendo hapa duniani kama wafanyavyo watakatifu mbunguni.

3. Mkristu yampasa kuondoa katika moyo wake mafadhaiko yote, na kila wasiwasi na mahangaiko na mashaka na tashwishi, hata kama mahangaiko hayo yanaonekana kana kwamba ni kwa ajili ya manufaa ya kanisa la Yesu Kristu. Wala asijidanganye mwenyewe kwamba anaweza kulinusuru Kanisa na mabaya yanayolokabili kabla hajajua vizuri nini ni mapenzi ya Bwana juu ya suala zima. Ni lazima

atie maanani kwamba Yesu Kristu pekee ndio kiongozi wa Kanisa lake na kwamba hakuna kitu kinachomchukiza na kuonekana hakina thamani kwake endapo mfuasi kwa kiburi na majivuno anadhani kuwa kwa uwezo wake mwenyewe analitendea Kanisa jambo jema. Kana kwamba mkombozi alihitaji ushirikiano na msaada wa ipofu kama hao. Hakuna hata mtu ambaye ni muhimu zaidi kwa ajili ya Utukufu wa Kanisa na ukombozi wa wanadamu kutoka katika utumwa wa dhambi. Ni kwa huruma ya Mungu tu itolewayo bure, kwamba alichagua kuwakweza wachache aliowakomboa akiwatumia, kama ilivyo sheria, wale walio dhaifu kabisa katika macho ya dunia, wale waliodharauliwa kabisa, ili waendeleze mpango wake.

4. Kwa kuhitimisha, na kujumlisha yote ambayo yamesemwa kuhusu lengo ambalo Mkristu anapaswa kujiwekea, na kulitilia maanani katika kila kitu anachofanya; tumeshaona kwamba anachopaswa kulenga, kwanza, ni utakatifu, ambao wenyewe tu unampatia Mungu sifa; pili ni kulenga juu ya Kanisa la Yesu Kristu kama njia iliyoteuliwa na Mungu kujiletea utukufu. Na Tatu: Wito wa Yesu Kristu, kama mtawala mapenzi yake, analialika Kanisa limpe Mungu utukufu Mkuu.

## Angalisho

Akishatakasa malengo yake kwa jinsi hii na kujichagulia *lengo* kuu katika mambo yote anayofanya kama ilivyoelezwa katika kanuni tatu hapo juu, mfuasi wa Yesu Kristu lazima ajue na kuamua kuhusu *njia* atakayotumia kufika lengo analolitamani. Atayavumbua haya kwa kuyaongoza maisha yake kufuatana na Kanuni tatu zilizopo katika mafundisho yanayofuata.

## Kanuni ya Nne

## *Kujiweka Kabisa na Kikamilifu katika Mpango na Maongozi ya Mungu*

1. Inawezekana ikawa hakuna kanuni nyingine zaidi ya hii inayoweza kusaidia kuleta amani ya rohoni, utulivu na uimara wa akili katika maisha ya Ukristu.

2. Kanuni hii ikitumiwa kwa unyofu wa moyo kama inavyoalika, inapita pengine nyingine zote katika kumfanya mfuasi wa Kristu, ampendeze saidi Baba wa Mbinguni. Kanuni hii inamwalika mfuasi wa Kristu kujiaminisha na kujikabidhi kwa Baba na kujiweka katika mapenzi ya Mungu. Kanuni hii inahitaji imani hai ambayo itamwongoza Mkristu, kuamini kwa uhakika kwamba mambo yote ya kidunia yawe makubwa au madogo, yamo mikononi mwa Mungu, na atatenda tu kufuatana na matashi ya Mungu ili kufikia malengo yake matukufu. Zaidi pia inadokeza imani katika wema usiopimika, ukarimu, ufadhili na huruma ya Baba wa Mbinguni. Baba wa Mbinguni anapanga kila kitu kwa manufaa ya wale wanaomwamini. Zawadi zake fadhila zake, rehema zake na matunzo yake yanatolewa kwa uwiano wa matumaini walio nayo watoto wake wapendwa.

3. Hakuna kanuni au mwongozo mwingine zaidi ya huu ambao Bwana wetu ameupendekeza kwa maneno na mifano yake. Ifuatayo ni hotuba aliyoitoa kwa wafuasi wake akiwapa moyo kufuatia mateso watakayopata mbele ya maliwali na wenye mamlaka. «*Nami nwaambieni ninyi rafiki zangu, msiwaogope hao wauao mwili, kisha*

*baada ya hayo hawana wawezalo kulitenda zaidi. Lakini nitawaonya, mtakayemuogopa, mwogopeni yule ambaye akiisha kumwua mtu ana uwezo wa kumtupa katika Jehanamu; naam, nawaambia, mwogopeni huyo. Je, mashomoro watano hawauzwi kwa senti mbili? Wala hawasahauliwi hata mmojawapo mbele za Mungu. Lakini hata nyewele za vichwa vyenu zimehesabiwa zote. Msiogope basi, bora ninyi kuliko mashomoro wengi. Akawamhia wanafunzi wake, Kwa sababu hiyo nawaambia, msisumbukie inaisha yenu, mtakula nini: wala miiili yenu, mtavaa nini. Kwa kuwa maisha ni zaidi ya chakula na mwili ni zaidi ya mavazi. Watafakarini kunguru, ya kwamba hawapandi, wala hawavuni; hawana ghala wala changa, na Mungu huwalisha. Bora ninyi mara nyingi kuliko ndege. Na yupi kwenu ambaye akijisumbua aweza kujiongeza kimo chake hata mkono mmoja? Basi ikiwa hamwezi hata neno hilo dogo, kwa nini kujisumbua kwa ajili ya yale mengine? Yatafakarini maua jinsi yameavyo; hayatendi kazi wala hayasokoti; nami nawaambia ya kwamba hata Sulemani katika fahari yake yote hakuvikwa vizuri kama mojawapo la hayo. Basi, ikiwa Mungu huvika hivi majani ya kondeni, yalipo leo na kesho hutupwa kalibuni, Je! hatawatendea ninyi zaidi enyi wa imani haba? Ninyi msitafute mtakavyokula wala mtakavyokunywa: wala msifanye wasiwasi kwa maana hayo yote ndiyo watafutayo mataifa ya duniani, lakini Baba yenu anajua kuwa mna haja na hayo. Bali utafuteni ufalme wa Mungu, na hayo mtaongezewa. Msiogope, enyi kundi dogo; kwa kuwa Baba yenu ameona vema kuwapa ule ufalme. Viuzeni mlivyo navyo mtoe sadaka. Jifanyieni mifuko isiyochakaa, akiba isiyopungua katika mbingu mahali pasopokaribia mwivi wala nondo haharibu. Kwa kuwa hazina yenu ilipo, ndipo na mioyo yenu itakapokuwapo»* (Lk 12:4-7, 22-34).

4. Jinsi gain yalivyo kamili haya mafundisho ya Bwana wetu yahusuyo kujitoa kabisa kwa mfuasi mwaminifu katika mikono ya Mungu.

5. Kutokana na mafundisho haya, mfuasi atajifunza kwanza, kwamba, Yesu Kristu ndiye msingi wa tumaini lake lote. Kwani anasema mwanzaoni kwamba anaowaambia maneno haya ni rafiki

zake. Na kwa neno "rafiki" hamaanishi wale tu ambao wako tayari wakamilifu bali anamaanisha Wakristu wote hata wenye dhambi. Rafiki zake hao aliowatendea jinsi hii, aliowafanya waelewe habari njema ya wokovu yaani Injili. Wote tunaweza tukapata faraja kutokana na wazo kwamba Yesu hakukataa jina rafiki hata kwa Yuda Iskarioti alipokuja kumsaliti. Ilihali tunamwamini Yesu, tunawo ndani yake, tunao msingi wa matumaini kamili kwa Baba yetu wa Mbinguni ambao hata dhambi zetu haziwezi kulipunguza.

6. Pili, Mkristu anajifunza kwamba jinsi ilivyo busara kujiweka kabisa katika uwema wa Mungu, ndivyo ilivyo upumbavu kujiamini nafsi yake mwenyewe. Kwani binadamu ni dhaifu sana, na hana uwezo wowote wa kubadili hata kitu kidogo kabisa katika mpango wa Mungu kwa vitu vyote katika ulimwengu. Mafanikio yake yote, uwepo na uhai wake, upo mikononi mwa Mungu; na hawezi kukwepa mikono hiyo hata akifanya nini, hata akienda wapi, hata angepanda mbinguni juu, hata angeshuka chini kuzimu.

7. Tatu, atajifunza kwamba, kufuatana na kuwa na mazingira haya ya matumaini kwa Baba wa Mbinguni, Mkristu hana haja ya kuogopa hata kidogo kuacha mambo yote ya kibinadamu, kwa kuuza vyote alivyo navyo na kuwapa maskini, kwa kukiri na kuungama umaskini ili ajitoe nafsi yake kabisa kwa mambo ya Mungu, akijitolea mwenyewe kwa Mungu, kutafuta ufalme na utakatifu, akiondoa moyoni mwake vifungo vyote vya kidunia – kwa kifupi, kumfuata Kristu, na kujifunga mwenyewe kwenye mti mtupu wa Msalaba wake Mtakatifu, akiifia dunia, na kuishi kwa ajili ya Mbingu tu. Kwani hazina yake ilipo na moyo wake ndipo utakapokuwepo pia.

8. Nne, anajifunza kwamba ingawa anakatazwa kuwa na woga wa mambo yasiyojulikana, mambo ya kibinadamu, anashauriwa ajivue mwenyewe kabisa kutoka katika mambo hayo Hata hivyo hajakatazwa kumwomba Baba yake wa Mbinguni kwa ajili ya mahitaji yake, kama ikiwa anafanya hivyo baada tu ya kuomba ufalme na utakatifu wake, na kwa minajili ya haya. Kwa hiyo mkate

wa kila siku tunaomba unaweza kusemwa kwa jinsi yoyote kwamba ni zaidi ya "chakula cha mwili". Hivo kwamba hii pia ni njia ya kutupatia baraka za kirohoni.

9. «*Ombeni nanyi mtapewa* – asema Bwana wetu – *tafuteni nanyi mtaona; bisheni nanyi mtafunguliwa; kwa maana kila aombaye hupokea; naye atafutaye huona; naye abishaye atafunguliwa. Au kuna mtu yupi kwenu, ambaye mwanawe akimwomba makate, atampa jiwe? Au akiomba samaki atampa nyoka? Basi ikiwa ninyi, mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! si zaidi sana Baba yenu aliye Mbinguni atwapa mema wao wamwombao?*». (Mt 7:7–11).

10. Maneno haya yanamfundisha Mkristu kuomba vitu vyote kwa Baba yake wa mbinguni akiwa na unyenyekevu na matumaini makuu, na kumfungulia yeye tamaa zote za moyo wake ilihali anafanya hivo kwa ombi moja tu; kwamba kila kinachompendeza Mungu kifanyike. Kwa kufanya hivi ataona matunda katika sala yake, kwa sababu Mungu atamsikiliza hakika, lakini wakati huo huo atasahihishwa na Mungu kutokujua na kutokufahamu kwake ikiwa anaomba vitu ambavyo aidha vinadhuru au visivyofaa na atajibu sala yake kwa kumpatia mafaa ya kweli yanayozidi maombi yake. Kwani yeye ni Baba anayejua kutoa vipawa vyema kwa watoto wake; kamwe hatoi vipawa vinavyodhuru.

11. Tano, Mkristu anajifunza kwamba, hakatazwi kufanya mambo yote ambayo kutokana na mipango asilia yanatosheleza mahitaji ya maisha. Anachokatazwa ni mashaka na wasiwasi kwa ajili ya vitu anavyokosa vinavyomasababishia mahangaiko ya moyo, na hivyo kuharibu amani ya roho na utulivu wa wale wamtegemeao Mungu kikamilifu. Katika hali iliyopo anaweza akaona mpango wa Mungu, na akafurahia vitu alivyo navyo kwa umaskini wa Roho na shukrani; lakini kilicho kinyume na kujitoa kabisa kufuatia mpango wa Mungu ni kule kuwa na woga (wa mambo yasiyojulikana) na kujali kuhusu wakati ujao (mambo ya kesho) kwani kuhusu hili mpango wa Mungu bado haujawekwa wazi na ni mpango wa

Mungu tu anaopaswa kupenda. Na ataonyesha upendo huo kwa kutumia na kufurahia, kwa kiasi na bila makosa, vitu alivyo navyo sasa, kwa sababu amepwea vitu hivi na Mungu. Lakini hasikii kufadhaika ama kukerwa kuhusu mambo yake kuhusu mambo hayo. Na kwa kuwa ni mpango huu wa Mungu ndio anaopenda, basi bado atafurahi tu akiwa amenyimwa mambo hayo, kana kwamba amepewa ikiwa kama Mungu amepanga.

12. Kwa sababu hii Yesu anasema pia «*(Bali) utafuteni kwanza ufalme wake na haki yake, na hayo yote mtazidishiwa. Basi msisumbukie ya kesho; kwa kuwa kesho itajisumbukia yenyewe. Yatosha kwa siku maovu yake*» (Mt 6:33-34). Kwa maneno mengine tusiache mahangaiko kuhusu kesho yaongeze madoa kwenye dhamira zetu ambazo tayari zimepata madoa kwa ajili wasiwasi kuhusu ya leo.

13. Kwa kifupi, njia ya uhakika ambayo kwa Mkristu anaweza kuchunguza kama amepungukiwa katika matumaini kamili anayoambiwa awe nayo katika uangalizi wa Baba yake wa Mbinguni, ni kwa kujichunguza na kuona kama katika moyuo wake anasikia mfadhaiko, kukerwa au wasiwasi juu ya vitu vyema na vibaya hapa duniani; kama ana amani moyoni mara zote, na kuridhika kabisa, na kuwa tayari kwa kitu chochote kinachoweza kutokea. Atagundua, pia kuwa tayari kwa kitu chochote kinachoweza kutokea. Atagundua, pia kama anapendelea kuwa na mashaka, huzuni, kama anasikia wasiwasi na mahangaiko kuhusu matokeo ya mipango yake; kama ni mtu wa imani haba, aliyegawanyika (chanika) kati ya matumaini na woga, wasiwasi, kila mara akisitasita, akitangatanga kuendelea kuwa na kigeugeu.

14. Sita, kwa kuwa ukamilifu wa Mkristu umo katika azma kamili ya kutotaka kingine chochote isipokuwa kile tu kinachopendeza zaidi kwa Mungu na kinacholingana zaidi na mpango wa Mungu, na kwa vile maisha haya ya ukamilifu si mengine bali ni kujitoa kabisa katika kumtolea Mungu utumishi kadiri inavyowezekana (kumtumikia Mungu kabisa) inafuata

kwamba, hata katika mambo ya kawaida anayofanya katika maisha ya kila siku, na katika kutumia na kufurahia mafao anayopewa na Mungu, anafanya mambo yote sio kwa faida au furaha yake mwenyewe lakini ni kw matumaini na ari kwamba katika mazingira hayo, hicho ndicho kinachompendeza Mungu zaidi (huko ndio kunakompendeza Mungu zaidi) na hivyo ndio kitu ana jambo kamili la kufanya.

15. Kwa hiyo, kwa kifupi, Mkristu makamilifu hafanyi mabadiliko katika maisha yake eti kwa sababu ya kuridhika kwake sasa, hata ikiwa katika mambo ambayo kimaadili yanakubalika, ila kwa sababu tu kufuatilia lengo lake moja – kutimiza wajibu wake na kuwa wa kupendeza zaidi mbele ya Mungu.

16. Kuishi kufuatana na kanuni hii kunaleta uimara, uthabiti, na uhodari ambao ni silika na tabia ya Mkristu mkamilifu katika hali yoyote atakayojikuta, iwe ni ya unyonge au ya uchangamfu kiatika maisha ya kiroho hatafuti mabadiliko, anabakia mwenye furaha na kuridhika, tena bila kuwa na mawazo ya kubadilisha hali hiyo isipokuwa kama imewekwa wazi kuwa ndivyo Mungu anavyotaka. Kawaida ya watu wote ulimwenguni ni kuwa hawatosheki na mapato yao katika maisha. Binadamu mara zote analilia kupata hali na nafasi ya juu na ubora zaidi katika maisha. Mara kadhaa hali hii inasababisha mafarakano na kutowatendea wengine haki. Ukamilifu wa Mkristu uanahitaji kila mmoja aridhike na hali aliyo nayo na kutimiza wajibu na majukumu aliyonayo katika jamii. Kwa Mkristu anayetafuta ukamilifu, mambo yote ni sawa kwake, ili mradi kwamba, anakuwa wa thamani mbele za Mungu, na anatimiza mapenzi ya Mungu ambaye anaona na kujalia yote.

17. Mwenendo na msimamo huu wa Mkristu katika hali yoyote anayojikuta, umfanya mtu kujua kinaga ubaga na kupenda majukumu na madaraka yake na namna ya kuyatimiza. Mwongozo huu ndio unaofaa zaidi ndio unaolingana na tabia na maumbile ya kibinadamu. Mtume Paulo katika kusizitiza hili anawaandikia

Wakorinto: «*Ndugu zangu, kila mtu na akae mbele za Mungu katika hali hiyo alivyoitwa nayo. Kwa habari za wanawali sina amri ya Bwana, lakini natoa shauri langu, mimi niliyejaliwa kwa rehema za Bwana kuwa mwaminifu – Basi naona hili kuwa jema, kwa ajili ya shida iliyopo kwamba ni vema mtu akae kama alivyo. Je umefungwa kwa mke? Usitake kufunguliwa. Umnefunguliwa? Usitafute mke. Lakini kama ukioa huna hatia; wala mwanamwali akiolewa hana hatia; lakini watu kama hao watakuwa na dhiki katika mwili, nami nataka kuwazuilia hayo. Lakini ndugu nasema hivi muda ubakiao si mwingi, basi tokea sasa wale walio na wake na wawe kama hawana; na wale walio kama hawalii na wale wafurahio kama hawafurahii; na wale wanunuao kama hawana kitu, na wale wautumiao ulimwengu huu, kana hawautumii sana kwa maana mambo ya ulimwengu huu yapita. Lakini nataka msiwe na masumbufu. Yeye asiyeoa hujishughulisha na mambo ya Bwana, ampendezeje Bwana*» (1Kor 7:24-32).

18. Saba, na ya mwisho, Mkristu anayeongozwa na kanuni hizi za utendaji, pia atakuwa tayari na mwenye kuridhika kufanya mabadiliko wakati mapenzi ya Mungu yanapofunuliwa kwake, au yale ya wakuu na wakubwa wake wanaoshika nafasi ya Mungu. Akili yake na mtazamo wake utakuwa mara zote umeandaliwa tayari kufuatana na ile kanunu ya dhahabu ya "kutokujali" iliyopendekezwa sana na mtakatifu Inyasi wa Loyola, aliyeifanya msingi wa mazoezi yake ya kiroho na hivyo wa maisha yote ya kiroho.

19. Hali hii ya "kutokujali" inatoka katika lengo sio tu la kumtumikia Mungu – lengo ambalo kwalo kila binadamu ameumbwa – bali pia kumtumikia yeye katika njia anayotaka kutumikiwa na kila mmoja wetu: na "kutokujali" kunabeba njia kuu ya kufikia ukamilifu.

20. Mkristu ambaye anataka kumtumikia Mungu sio kwa jinsi anavyotaka mwenyewe bali kwa jinsi anavyotaka na anavyoonyesha Mungu atafikia "kutokujali", kwa kadri uhuru wake unayehusika, ingawa si lazima kufuata mivuto ya maumbile, kufuatia hatua nne za

hali zilizoainishwa vizuri na mtakatifu Inyasi, kwanza, kutokujali iwe kwa afya nzuri au ugonjwa, pili iwe kwa utajiri na raha au kwa umasikini wa maisha, tatu kwa heshima au madharau ulimwengu, nne kwa maisha marefu au mafupi, hata kama yamefupishwa na kazi na mateso.

21. Kwa hiyo mfuasi wa Kristo atakuwa mara kwa mara anajichunguza mwenyewe ili aone kama amefikia kweli kutojali kuhusu umasikini au utajiri, heshima au madharau kuhusu afya njema au magonjwa, maisha marefu au mafupi; na kwa hii atagundua ni kwa kiasi gani amesonga mbele katika njia ya ukamilifu wa Injili.

22. Hali hii ya "kutokujali" ambayo Mkristo mwaminifu anapaswa kila mara kuikusudia inaweza kufupishwa katika sehemu tatu: "Kutokujali" kufuatia kazi yoyote atakayokabidhiwa: "kutokujali" kufuatia mahali popote anapopangiwa kuishi; na "kutokujali" kufuatia hali yake ya kiafya.

NB. "kutokujali" ni neno ambalo kwa kiingereza ni *Indifference*. Hapa pia linamaanisha "utayari".

## Juu ya Kanuni ya Tano

## *Kuungama, na Kukiri kwamba Mimi Si Kitu Mbele ya Mungu, ni Bure*

1. Mfuasi wa Kristo anapaswa aishi siku zote katika ule upweke na ukimya wa rohoni, ili kusudi afukuze mbali kutoka katika akili yake vitu vingine vyote, ili kusudi Roho wa Mungu weze kukaa ndani mwake.

2. Yampasa kuwa na Mungu katika akili yake mara zote aweze kuabudu ukuu wa Mungu, na lazima ajifahamu yeye mwenyewe ili aweze kuona na kuelewa kwa uwazi zaidi juu ya mapungufu yake na "ubure wake".

3. Mkristo anatakiwa awe ameshawishiwa na kukubali kwa undani juu vigezo vinavyothibitisha huu Ubure vigezo vile vinavothibitisha ubure na umaskini wa vitu vyote vilivyoumbwa; vile ambayo hasa vinamnyenyekesha mwanadamu na vile vinavyomnyenyekesha nafsi yake mwenyewe.

4. Kama jinsi alivyo kama chembe au nukta akilinganishwa na ulimwengu ndivyo alivyo kama si kitu akilinganishwa na Mungu, ambaye ni asili ya kila kitu kilicho chema alicho nacho wanadamu. Dhambi ambayo katika hiyo alituungwa miiba, tabia na mvuto wake wa kupenda kuelekea mabaya pamoja na dhambi ambazo kwazo ameichafua roho yake lazima imjulishe na kumsadikisha kuhusu dhana mbili za ukweli ufuaao kwanza: kuhusu yeye mwenyewe kutokuwa na uwezo wa kufanya jambo lolote jema, pili sio kitu

kwamba anaweza kuanguka dhambini, bali pia yuko dhaifu kiasi kwamba wakati wowote anaweza kuanguka dhambini isipokuwa pale tu ambapo Mungu ataonyesha huruma yake. Ndio maana kulingana ma maneno ya Mtume Paulo, Mkristu anapashwa kuufanyia kazi wokovu wake mwenyewe kwa kuogopa na kutetemeka (Fal 2:12).

5. Ya kwanza katika ya hizo mbili za ukweli itamshawishi ili asichaguue kufanya shughuli (kitu chochote) yeyote, isipokuwa kama anavutwa kufanya hivyo kwa kujua kwamba haya ndio mapenzi ya Mungu. Hii haihusu tu mabadiliko katika nafsi yake katika maisha (kama ambavyo imekwishaelezwa) lakini pia kuhusu mambo yeyote mengine kama mtu anasadiki kweli kwamba hawezi kufanya lolote zuri kwa matakwa yake huku akijua kuwa hana uwezo wa kufanyalolote lililo jema bila msaada wa Mungu.

6. Mambo mawili yanayopingana ambayo ni hali halisi inayokubalika lazima yajitokeze ndani ya Mkristo peyote. Atakuwa na ari kubwa kwa ajili ya utukufu wa Mungu na wema kwa jirani yake sambaba na sauti inayomwambia kuwa yeye kwa nafsi yake hana uwezo wa kufanya lolote jema wala nguvu ya kuepusha maovu yanayotokea duniani.

7. Kwa hiyo ni lazima aige unyenyekevu wa Musa, ambaye hakuweza kuamini kirahisi kuwa ni yeye alichaguliwa kuwaweka huru watu wa Mungu. Kwa sababu hiyo, kwa upendo wa upole na kwa matumaini alizungumza na Mungu akiomba aachwe asifanye hiyo kazi kwa sababu alikuwa siyo mzungumzaji mzuri, alikuwa na kigugumizi. Alimwomba Mungu badala yake atumwe yeye ambaye aliahidiwa – yaani Mashiha. Na alifanya hivi bila kujali juhudi na hamu yake binafsi juu ya ukombozi wa wate wake. Hivi pia Mkristu anapaswa aendelee kutafakari na kuiga unyenyekevu wa Mama Bikira Maria. Tunamuona katika maandiko alielezewa kama mkunjufu, safi, mtulivu na mwenye amani. Kwa uchaguzi wake mwenyewe aliishi maisha ya unyenyekevu, asiyetaka makuu wala

fahari, maisha ya ukimya na faragha. Na alivutwa kufanya hivi na shauti ya Mungu wenyewe tu au kwa hisia za mapenzi kwa binadamu yake, Elizabeti. Nani angetegemea kwamba kungekuwa na mambo machache hivi yaliyandikwa katika maandiko kuhusu aliye mkamilifu zaidi ya binadamu wote? Hatusikii habari yoyote ya kazi aliyofanya. Ulimwengu wa giza ungeyaita maisha yake maisha ya uvivu. Hata hivyo Mungu ameyatangaza maisha hayo kuwa maisha ya juu sana, maisha bora sana, maisha mema na ya maadilifu kuliko maisha mengine yote. Matokeo yake, Mungu alimwinua mwanamke huyu mpole na mdogo, asiyejulikana na kumpa heshima ya hali yajuu na kumvika taji la utukufu ambalo hajapata kupewa binadamu mwingine popote duniani wala malaika mbinguni!

8. Ukweli mwingine wa pili ni ule wa kwamba Mkristo lazima aogope hatari zilizojaa ulimwenguni kwa kadiri ya mafundiho ya Maandiko Matakatifu. Mtakatifu Yahana Mwinjili anathubutu kutuambia kwamba kuwa kila kitu dunia ni hatari

9. Kwa sababu hizi, Mkristo anayetafuta ukamilifu ataishi maisha ya kujitenga, utauwa, ya ukimya na ya kujishughulisha kila wakati.

10. Upweke wa Mkristu utazingatia uamuzi wake wa kutotoka nje ya makazi yake bila sababu maalumu, labda iwe kwa mujibu wa majukumu ya wajibu wake au kwa ajili ya mahitaji ya upendo kwa jirani yake.

11. Atajifunza na kujizoeza ukimya akikwepa maneno yasiyo na maana, ndiyo kusema, maneno ambayo hayamjengi yeye wala kuwajenga wengine au hayatakikani kulingana na shughuli au mahitaji ya maisha yake.

12. Mwisho, atajishughulisha mwenyewe kila wakati kuhakikisha kwamba hata mara moja hatakubali kupoteza muda. Atakuwa mara kwa mara akitafakari kwamba muda ni kitu cha

thamani sana; na kwamba haiwezekani kufidia muda tuliopotea bila kupata mafao ya kiroho; na pia kwamba tutawajika kutoa hesabu ya kila dakika ya huu wakati, kama vile ya talanta tulizokabidhiwa tuzishughulikie. Mtazamo huu kuhusu muda ni wa lazima kwa yule anayetafuta ukamilifu. Kwa dhumuni hili mtu anajiandaa mwenyewe ili ahudhurie kadiri atakavyoweza kwenye kumwabudu Mungu peke yake, hivyo basi lazima atolee nguvu zake zote na muda wake wote kwa ajili hiyo.

## Juu ya Kanuni ya Sita
## *Kuyaongoza Matendo yote ya Maisha kwa Roho wa Ufahamu (Roho wa Akili)*

1. Mkristu ni lazima atembee katika mwanga siku zote, na kamwe sio gizani.

2. Kwa sababu hiyo, Mkristo hana budi kusali bila kuchoka kumwomba Roho mtakatifu karama ya Akili ya kupambana na kuelewa ukweli juu ya imani: paji la Hekima ambalo kwalo atawezeshwa kuamua kwa busara kuhusu mambo ya Kimungu; paji la Elimu ambalo kwalo atawezeshywa kuamua vema juu ya mambo ya kibinadamu. Na mwisho paji la Shauri itakalomwezesha kuyaongoza mambo yake ya binafsi, akitumia dhana mbalimbali za ukweli alizojifunza katika mazingira ya maisha.

3. Mkristo lazima atamblike kwa fikira, busara, busara na ukomavu wake ambavyo vitajitokeza na kuonekana katika nyanja zake zote za maisha. Anapaswa kujiepusha na pupa na haraka haraka zisizo na busara ambavyo ni tabia za watu wa dunia, kwani hivi vinapingana mapaji yaliyotajwa hapo juu. Pupa na haraka haraka ni tabia za binadamu mwenye wasi wasi. Hivi huharibu amani na utulivi wa rohoni uliopendekezwa na Bwana Wetu Yesu Kristu.

4. Roho wa akili atamuongoza Mkristo kila mara kutoa boriti katika jicho lake mwenyewe kabla ya kutoa kibanzi katika jicho la jirani yake.

5. Kuhusu marekebisho na ukamilifu wa maisha yake, mapenzi ya Mungu yatafunuliwa kwa urahisi kwake, na atayaona mapenzi ya Mungu katika mazingira atakayojikuta. Kufuatana na kanuni hii atafahamu: Kwanza, kwamba jukumu, wajibu wa kwanza ambao mapenzi ya Mungu yanamtaka afanye ni kufanya kwa uaminifu, kwa uhakika, kwa wepesi, uhodari na kwa wakati ule ule, shughuli zote zinazotokana na uhusiano wake na watu wengine; na kuwaonyesha ukarimu, upole na wema unaotokana na uhusiano huo. Kwa kifupi anapaswa kuonysha upendo kiasi kwamba watependezwa naye. Hivyo pia akiwa anashughulikia watu wengine (na kutokana na upendo wake kwa faragha, usio wa kujionyesa atakwepa shughuli ambazo hazimlazimu). Mwenendo, matendo, na tabia yake vitakuwa kwa upole wa urafiki kiasi cha kujenga na kuigwa na watu wengine.

6. Kanuni hiyo hiyo ya kutimiza wajibu wake kadiri alivyojaliwa na Mungu na kwa kutumia muda wake vizuri, kutamfanya apende kufanya kazi kwa bidii na hasa kazi zile ambazo ni za taaluma yake na atazifanya kwa uadilifu. Kama atakuwa na maendeleo yoyote katik kazi hizo ataona kuwa ni upendeleo toka kwa Mungu kwani ni kwa kadiri ya mapenzi ya Mungu afanye vizuri na afaulu katika yote.

7. Kama muda wa Mkristu ni kwa ajili ya kujielimisha, atafanya hivyo na kuendelea kujifunza siyo kwa ajili yake mwenyewe, bali kwa ajili ya mapenzi ya Mungu ambaye pekee anamtumikia. Huu ndio wito wake kwa wakati huo na anapaswa kufanya hilo kwa nguvu zake zote, kwa akili yake yote na kwa roho yake yote. Kama amepewa kazi za mikono au za kiufundi, atazifanya kazi hizo kwa bidii kwa lengo hilo hilo. Kwa hiyo Mkristo mkamilifu hatajagua au kubagua kazi, kuwa hii ni bora na ile ni duni kwani kazi zote zipo kwa ajili ya kumtukuza Mungu. Mwisho wa siku wote tutapokea ujira siyo kwa aina ya kazi tuliyofanya, bali kwa jinsi tulivyofanya kazi hizo kwa uaminifu, uadilifu na uangalifu mkubwa ambavyo kwavyo tumempendeza Bwana na siyo binadamu.

8. Ikiwa mfuasi wa Kristo ametimiza wajibu katika hali na nafasi yake katika jamii, ikiwa ni pamoja na wajibu wake wa kidini, atatenga muda kwa ajili ya kusoma masomo ya kiroho na kwa ajili ya sala. Kwa kusoma vitabu juu ya imani yake atajiongezea elimu juu ya imani na kutafakari ukuu na wema wa Mungu usiopimika na wa milele, atajua zaidi utakatifu na hekima ya Mungu. Atatenga muda wa ziada kwa ajili ya sala za binafsi pengine hata awapo sehemu yake ya kazi. Lazima aijue sala na kuipenda. Na kwa kweli aipende sala zidi kuliko yote na kuutumia muda wa sala kama muda wa furaha na wa neema. Kwa sababu licha ya kuwa mtu hana stahili yoyote, kwa njia ya sala anakaribushwa mbele ya Mungu na kuruhusiwa kuongea naye moja kwa moja na kwa faragha.

9. Mkristo augawe muda wake kwa ajili ya mahitaji ya kimwili, kwanza kwa ajili ya kula na kupumzika. Chakula chake kiwe cha kiasi, cha kawaida na kinachobuirudisha. Muda wa kupumzika pia uwe wa kiasi.

10. Pia atenge muda wa kupumzika wakati anapochoka. Yesu Kristo ametuachia mfano wa kufanya mambo yanayolinda miili yetu ikiwa na pamoja na kupumzika pale mwenyewe alipolala mtumbwini na lipokaa kando ya kisima cha Samaria.

11. Mazingira atakayojikuta na mahusiano yake na watu wengine yawe kiasi kwamba haoni aibu wala kujitenganisha na mashauri ya kiinjili ambayo ni nadhiri zake za ufukara, usafi wa moyo na utii. Kwa hiyo, Mkristo ambaye anatamani sana wakati wote kuwa mfano wa Kristo kadiri inavyowezekana na kutopuuza jambo lolote alilojaliwa na Mungu kuwa ndiyo maisha ya ukamilifu, ataishi maisha ya kiinjili kwa ujasiri na kwa moyo mkuu. Kama ana uwezo wa kufanya hivyo basi ataish kwa kadri ya nadhiri zote tatu, vinginevyo ataishi nadhiri moja au mbili kulingana na hali yake na mazingira yanavyoruhusu.

12. Mkristo hajitafutii kwa uwezo wake mwenyewe kufanya

mambo makubwa, maana anajua kuwa hana uwezo wa kufanya lolote jema isipokuwa kwa neema ya Mungu. Ingawa anaridhika kujitoa kabisa katika kutimiza wajibu wake kwa taifa na serikali daima akumbuke kuwa amechagua maisha ya upweke, ukumya na kutojlikana. Pamoja na hayo, haina maana kwamba hahusiki kuhusu maendeleo, maafa na majanga ya watu wanaomzunguka. Atawaombea, atawatakia mema kutoka moyoni na atakuwa kwa wakati wote tayari kujikatalia kwa ajili ya wengine, kutumia bidii zake zote kwa mafaa yao ya kiroho, akisadiki na kuamini kuwa anachokifanya kwa ajili yao hakikutonana wala kuanzishwa na ujasiri au matakwa yake mwenyewe bali ni matakwa ya Mungu yanayomtaka afanye hivyo.

13. Roho wa ufahamu pia anatakiwa kumwongoza Mkristo kuhusiana na kufahamu mapenzi ya Mungu na anafyopaswa kuwahudumia jirani zake.

14. Huyu roho wa ufahamu anamfundisha Mkristo kwamba katika wajibu wake wa kuwahudumia jirani zake, yaani matendo ya huruma kwa wenzake, mapenzi ya Mungu kwa kawaida na kwa kiasi kikubwa yanafunuliwa kwake katika mazingira ya nje na ya kawaida. Haya Mazingira, ambayo kwayo ataweza kwa usalama kufahamu ni aina gani maalumu ya kazi za huruma anaitwa kufanya kwa jirani yake ni kama ifuatavyo:

a) Wakati anapoweza kuona kwa macho yake mwenyewe mahitaji ya jirani yake, kama navyosemwa na Mtakatifu Yohane waziwazi. «*Lakini mtu akiwa na riziki ya dunia, kisha akamwona ndugu yake ni mhitaji, akamzuilia huruma zake, je! Upendo Mungu wakaaje ndani yake huyo?*» (1Yoh 3:17).

b) Wakati anapoombwa na jirani yake amfanyie huduma fulani huruma kama Bwana wetu katika sehemu nyingine anavyosema: «*Basi ninyi mtakuwa wakamilifu kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu*» (Mt 5:48): Na katika

sehemu nyingine tunaambiwa kwamba Baba yetu wa mbinguni atatupa kila tumwombacho katika jina lake Yesu (Yoh 16:23). Hivyo pia, Mkristo lazima kujitoa kwa jirani yake kadiri awezavyo kufuatia maombi ya jirani, kama anataka kuwa mkamilifu kama Baba yake wa mbinguni alivyo mkamilifu

16. Kama anakusudia kuwa mwaminifu katika wito wake wa kuishi maisha ya ukamilifu wa upendo, Mkristo yampasa kufanya kazi yoyote anayoitiwa na ambayo anajua ni mapenzi ya Mungu kwa moyo mkunjufu na kwa furaha. Aifanye hiyo hata kama italeta usumbufu mkubwa kwake au itakuwa kwake sadaka, kwa ufupi, «*Kila mtu asiangalie mambo yake mwenyewe, bali kila mtu aangalie mambo ya wengine*» (Fal 2:4). Huu ndio upendo ambao Bwana wetu Yesu Kristo aliwafanyia wanadamu wote, upendo usiojua mipaka uliofikia hata Yeye kumwagwa kwa damu Yake msalabani.

17. Hivi ndiyo itakavyokuwa kwa Mkristo mpole na mwenye bidii, ambaye yeye mwenyewe hawezi kufika kuchagua kitu chochote isipokuwa maisha ya kutojionyesha. Maisha ya kuuepuka hatari za dunia, maisha ya kuzama katika tafanario yaliyogawanyika katika sala na kujifunza, ua kufanya kazi ya kitaalamu kazi fulani ya mikono (ya nguvu) akishughulikia mahitaji yake ya maisha, pamoja na muda mchache wa mapumziko, maburidisho, michezo. Atavutwa aache maisha yake ya upweke – anayoyapenda sio kwa uvivu, uzembe, au ulevi, bali kwa ajili ya upole wa kweli – na ataongozwa kufuata maisha ya Injili, maisha ya utendaji, labda ikiwa Mungu anapenda, maisha yatakayomtumbukuza katika kilindi cha kutunza bahari ya matatizo ya biashara na shughuli za kila aina, kubwa au ndogo za heshima au za madharau, kwa ajilli ya jirani yake kufuatana na mapenzi ya Mungu na atapokea aina yoyote ya kazi kufuatana na mpangilio wa mapenzi ya Mungu yanavyojitokeza kwake.

18. Akiongozwa na huyo roho wa ufahamu, Mkristo aliyejawa na upendo atajitokeza katika tukio lolote. Kwa hiyo atachukulia

kufanya vitu vikubwa, kazi ngumu na za hatari, kitu chochote kile ili mradi kwamba Mungu anampatia thibitisho la moyoni kwamba ni kazi iliyo ndani ya uwezo wake, na ilimradi kwamba wakubwa wake hawakatazi na anaombwa wazi au kwa kimya lakini iliyodhihirisha bila kusemwa na jirani yake, ambaye kwake anamuona Bwana Mungu.

19. Mkristo anayependa ukamilifu, atafanya kazi hizi za upendo bila kuwa na ubaguzi wa hiari wa kazi moja kuliko nyingine. Kupenda kwa hiari kuchagua kazi moja badala ya nyingine kwani hakuna kazi kubwa kuliko nyingine, ili mradi kila anatimiza mapenzi ya Mungu.

20. Kwa hiyo atazingatia sheria tatu zifuatazo;

a) Atachagua kazi za kwanza za upendo atakazoombwa kufanya na jirani yake; iwe ni kubwa au ndogo, za kufurahisha au kuelemea, kiasi kwamba mtu yeyote angeweza kufanya, au zinamfaa yeye tu, hatazikataa, kwa hoja kwamba, anangojea miito mingine isiyo wazi katika upendo wake.

b) Na kama akiombwa kufanya kazi kadhaa za upendo kwa wakati mmoja, wakati ule ule na akiona hataweza kuzifanya zote, atachagua kutoka katika hizi kufuatana na "mpango wa upendo" – akiwa mwangalifu mara zote ili asichague kazi iliyo zaidi ya uwezo wake.

c) Mwisho na kama atabanwa na kazi hizo au zinachukua muda wake mwingi na zinamfaya ashindwe kufanya kazi nyingine, atavumilia na kumaliza kazi zote alizoanza, akidumu katika kazi hizi kuliko kuchukua kazi nyingine kwani kwa wakati huo hizo ndizo kazi ambazo Mungu anamtaka azifanye.

21. Mapenzi ya Mungu, zaidi ya kujiweka wazi kufuatia mazingira ya nje, yanaweza kuwekwa wazi kupitia maongozi ya

ndani ya ki-Mungu ya kawaida. Lakini ni pake tu ambapo mazingira ya nje hayapingani kabisa na haya ya ndani.

22. Inaweza ikawa kwamba Mkristo, pamoja na kujua hali ya "ubure" wake atachukua kazi tofauti na zile zinazopendekezwa na hali yake, kupitia msukumo wa ndani kutoka kwa Roho Mtakatifu, ambao kwao mapenzi ya Mungu yanaonyeshwa wazi kwake.

23. Lakini msukumo wowote wa aina hii ni lazima ujaribiwe kweli kweli. Tunapaswa kuchunguza siri za mioyo yetu kuhakikisha kwamba pengine hatudanganywi na na ubinafsi na yule mwovu, ambaye wakati mwingine anajifanya kama malaika wa mwanga. Na mwisho ingekuwa vizuri kama msukumo huo ungethibitishwa na viongozi wetu wa kiroho au washauri wetu wa kiroho.

24. Kwa hiyo njia ya kawaida, sheira ya kawaida isiyokosea katika kufahamu mpango wa Mungu, mapenzi ya Mungu, iwe yamefunuliwa kupitia mazingira ya nje au kupitia msukumo wa moyoni, ni ile amani na utulivu wa rohoni ambao Mkristo anapata kuhusu mambo hayo ndani ya damira yake. Yampasa ajichunguze kwa makini na uangalifu na kuona kama anasikia mahangaiko ya moyo. Uchunguzi wa makini utaonyesha hali yake halisi. Pale ambavyo upendo binafsi upo au nia zozote za kibinadamu, mtu huyo kwa kawaida atasikia kiasi fulani cha mahangaiko. Na kama akigundua na kuhisi kitu chochote cha aina hii katika dhamira yake, anaweza kugundua mara moja chanzo chake kama anataka, na kuona kwamba chake hakitoki katika Roho kamili wa Mungu – Roho wa utulivu kamili lakini ndani katika roho yake mwenyewe, matokeo ya kiburi chenye hila, akili ya kibinadamu ambayo bado haijashinda. Kwa kifupi, mafunuo yake yatoka katika hila na Udananyifu wa adui.

25. Kama Wakristu wangezoea kufanya mambo haya yote, wakifuata na kuyaishi mafundisho ya Bwana wao, kwa pamoja wangefanya jumuiya yenye furaha na amani, sio tu kwa maisha yajayo, lakini hata katika maisha ya sasa.

# Nyongeza
# *Wasifu wa Mwenyeheri Padri Antonio Rosmini*

Habari za Antonio Rosmini ambaye alikuwa Padri, mwanafalsafa, mchungaji na mwanzilishi wa Shirika la Kitawa mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa, hazijulikani sana katika nchi zinazoongea lugha ya Kiingereza na Kiswahili. Hata hivyo katika nchi ya Italia na mahali Kiitaliano kinapozungumzwa, Antonio Rosmini anajulikana sana kama mmoja wa watu walioboresha maisha ya Kikatoliki katika nusu ya karne ya kumi na tisa na karne ya ishirini. Mnamo 1955, Raisi wa nchi ya Italia Bwana Gronchi, alituma ujumber rasmi kwa mkuu wa Shirika la Warosmini katika ya miaka mia ya kifo cha Rosmini, uliosema kwamba alikuwa miongoni mwa waanzilishi na mwanafalsafa mashuhuri kutoka Italia na Ulaya katika karne ya kumi na tisa. Licha ya kuwa mwanafalsafa na mwanasiasa, zaidi sana alikuwa mwalimu, siyo tu kwa mfano wa maisha yake bali pia kwa kupenya na kuelewa mioyo ya watu. Matendo yake ya kisomi na utu wake wa kitakatifu yaliyofika upeo mkubwa ndio yaliyoibua misingi ya fikra za Kikatoliki za nyakati zile.

## Antonio Rosmini ni nani?

Antonio Rosmini Serbati (kama alivyojulikana) alizaliwa 24.3.1797 katika mji mdogo wa Tyrol karibu na Rovereto kaskazini mwa Italia, sehemu iliyokuwa chini ya utawala wa nchi ya Austria wakati ule. Familia yake ilikuwa ya watu matajiri wakubwa waliomiliki vivanda vikubwa, naye alilelewa na kukua katika jumba

kubwa la kifalme. Vipaji vyake vikubwa vilianza kuonekana mapema akiwa na umri mdogo. Alipenda kusoma vitabu hata kabla hajaanza shule na hata kabla ya balehe alijua sana maandiko Matakatifu yaani Biblia aliyokuwa ameisoma kuanzia mwanzo hadi mwisho.

Akiwa bado mtoto aliwashangaza wengi wa wakati wake kwa vile mara nyingi alikuwa akishinda ndani ya kanisa la Parokia yake katika sala na vipindi virefu vya tafanario. Tayari alionekana kumpa Mungu nafasi katika maisha yake na alikuwa na masimamo thabiti juu ya kujitoa maisha yake kwa ajili ya huduma kwa Mungu kupitia wito wa Upadre.

Akiwa mtoto wa kwanza wa kiume wa familia yake, Rosmini alitegemewa kushika nafasi katika familia ya kifalme. Tayari palikuwa na matayarisho ya kupewa majukumu ya kijamii ambapo angefundishwa sanaa na muziki, miongoni mwa mambo mengine. Kwa ujasiri mkubwa aliwaambia wazazi wake kuwa Padre anahitaji kujufunza sanaa na muziki. Wakati huu alikuwa na umri wa miaka kumi na sita. Baada ya kuvutiwa na uwezo wake wa kielimu na kujifunza mambo mengi, mmoja wa waalimu wake alitabiri kuwa baadaye dunia itasikia habari zake Rosmini.

Kwa maneno hayo Rosmini alijibu kwa kusema kwamba shughuli zake za baadaye zitalenga kwenye jambo moja tu nalo ni kueneza utukufu wa Mungu kwa uwezo wake wote. Alitoa sababu ya kusema hivyo kwamba lengo la kila mtu hapa duniani ni kumpenda Mungu kwa moyo wote na kuwapenda binadamu wengine.

Akiwa na umri wa miaka kumi na tisa aliingia chuo kikuu cha Padua kwa sababu alinuia kuwa Padre. Pamoja na masomo ya upadre alihudhuria pia masomo mengine kama hisabati, kemia, elimu ya viungo, elimu ya madawa na kilimo. Akiwa na miaka ishirini alipokea kanzu. Wakati huo aliandika kuwa anasikia zaidi na zaidi sauti ya uhakika kuhusu wito wake wa kipadre na kwamba kila siku alikuwa akiimarika katika uamuzi wake wa kumtumikia Mungu kama Padre.

Baada ya kufariki baba yake mwaka 1820, wakati huo Rosmini akiwa na miaka ishirini na mitatu, alirithi sehemu kubwa ya mali ya

familia yake, kiasi cha theluthi mbili ya mali zote. Hata hivyo urithi huu haukumzuia kuendelea na nia yake ya kuwa Padre kwani mwaka 1821 alipata daraja la Upadre. Katika maadhimisho ya Misa Takatifu Rosmini alikuwa akitoa tafanario nzuri na ya kina zilizowavutia wengi. Hata Mt. John Bosco alisema waziwazi kuwa hajawahi kumwona Padre aliyeadhimisha Misa kwa tafanario kubwa kama ya Rosmini.

Baada ya Upadrisho Rosmini aliandika kwenye kumbukumbu yake: *kuanzia sasa lazima niwe mtu mpya, niishi mbinguni kwa moyo na akili zangu, daima niongee na Kristo, niachane na mambo ya dunia hii. Lazima siku zote niondoke altareni nikiwa mtakatifu, mfuasi, mtu aliyejawa nna Mungu, lazima niendelle katika ubora wote.*

Baada ya kufunuliwa na Mungu kwa njia ya mazingira na matukio mbalimbali katika maisha yake, Rosmini alianzisha Shirika la Mapendo mwaka 1828. Mwanzo wa Kwaresma ya mwaka 1828, Rosmini alikwenda katika mlima mmoja uliopo kaskazini mwa italia karibu na mji wa Domodossola, mlima uitwao Calvario. Huko alitumia muda wote wa Kwaresma katika sala akimwomba Mungu athibitishe mapenzi yake kwake. Wakati huo pia aliutumia kuandika katiba ya Shirika la Mapendo.

Mwaka 1830 Rosmini aliandika vitabu viwili, cha kwanza kinaitwa *Kanuni za Ukamilifu wa Kikristo* na cha pili kinaitwa *Insha Mpya juu ya Mwanzo wa Mwanzo*. Kitabu cha kwanza ndicho kilichoweka msingi wa Karama za Rosmini na karama za Shirika lake la Mapendo, wakati cha pili ndicho kilichoweka msingi wa falsafa ya Rosmini.

Rosmini aliliongoza Shirika lake la Mapendo tangu lilipoanzishwa hadi alipokufa tarehe 1 mwezi wa Saba mwaka 1855. Rosmini alikufa baada ya kuandika vitabu vingi katika nyanga mbalimbali, vingine vilipokelewa vizuri, vingine vilipata upinzani mkubwa hasa kile kinachoitwa, *Madonda Matano ya Kanisa Takatifu*.

Wakati wa mazishi ya Rosmini watu wengi waliandika rambirambi zao. Mmojawapo ni Askofu mmoja wa Uingereza aliyeitwa Ullathrone aliyesema: *kupotelewa na mtu mashuhuri na mwenye akili nyingi kama huyu lazima kunagusa mioyo ya wengi.*

*Yueye alikuwa mrejeshaji wa falsafa ya juu na ya kina inayotafuta kuoanisha ufuno na fikra, na inayojali mpango wa Mungu wa asili*. Naye John Henry Newman katika rambirambi zake aliongeza kusema juu ya Rosmini: Rosmini alikuwa mali ya Kanisa.

Katika kumbukumbu ya miaka 150 tangu kuzaliwa kwa Rosmini, Baba Mtakatifu Yohana Paulo II alisema: *Antonio Rosmini alikuwa mtu mashuhuri aliyejukikana kidogo hadi leo hii. Alikuwa msomi mashuhuri na mwenye hekima na aliandika jumla ya vitabu tisini na tatu vilivyojaa elimu ya nyanja nyingi, falsafa, maadili, siasa, dini, uchungaji, vitabu vinavyostahili kujulikana na kusambazwa mahali pengi duniani. Fikra za Rosmini na karama zake zinapaswe kujulikana na kuigwa na labda yeye mwenyewe angehesabiwa kuwa mlinzi huko mbinguni. Kwa hamu kubwa tunatazamia kuona siku ile mambo hayo yatakapotokea*. Hatimaye Rosmini alitangazwa Mwenyeheri na Baba Mtakatifu Benedicto wa kumi na sita 18.11.2007 huko Novara Italia na sikukuu yake inaadhimishwa siku ile alipozaliwa mara ya pili yaani alipoalikwa Mbinguni tarehe Moja July.

Shirika la Mapendo baada ya kuanzishwa Italia limeenea pia katika nchi za Uingereza, Ireland, USA, Venezuela, India, New Zealand, Kenya na Tanzania.

*Mwenyeheri Antonio Rosmini ameandika kitabu hiki kwa ajili ya Wakristu wote. Hivyo kitabu hiki kimedhamiria kwa wafuasi wote wa Yesu Kristu, na siyo kwa Watawa tu. Hii ni kwa sababu. kama asemavyo Antonio Rosmini «wote, katika hali yoyote ya maisha watakayojikuta wanaalikwa na Injili kuwa wakamilifu».*

*Kufikia ukamilifu Antonio Rosmini katika kitabu hiki ametupatia Maadili sita. matatu ya mwanzo ndiyo "lengo" na matatu ya mwisho ndiyo "njia" ya kufikia lengo.*